TANGAZO LA SERIKALI NA. 230 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# KANUNI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 37A(4))*

## KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UTOAJI NA USIMAMIZI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU ZA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 856 la 2024

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2025, na zitasomwa pamoja na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2024 ambazo hapa zimerejewa kama "Kanuni Kuu".

Marekebisho kanuni ya 6

2. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 6(1) kwa kuongeza maneno "katika ngazi ya kata au Wilaya" mara baada ya neno "ujasiriamali" lililopo katika aya (g).

Marekebisho ya kanuni ya 22

3. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 22(1), kwa-

(a) kufuta neno "na" katika aya (h);
(b) kuandika neno "na" mwishoni mwa aya (i); na
(c) kuongeza aya ifuatayo mara baada ya aya (i):
"(j) Mkuu wa Divisheni ya Kilimo na Mifugo.".

Marekebisho ya kanuni ya 29

4. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya kanuni ya 29 kama ifuatavyo:

"Wajibu wa Kamati ya Bajeti ya Halmashauri
Sura ya 439
TS Na. 336 la 2015

29.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Bajeti ambayo itaundwa kwa mujibu wa kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti na kanuni ya 17(3) ya Kanuni za Bajeti.

(2) Kamati ya Bajeti itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kutenga bajeti ya asilimia kumi ya mapato ya ndani yasiyolindwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi;
(b) kutenga fedha ya asilimia kumi ya mapato ya ndani yasiyolindwa kwa ajili ya mikopo ya vikundi; na
(c) kutathmini utekelezaji wa bajeti ya asilimia kumi.".

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*